

# **Utabiri wa hali ya hewa kwa kutumia programu ya mtandao**

Ili kufanikiwa na kilimo wakulima, hali ya hewa lazima iwe nzuri kwa ukuaji wa mazao katika msimu fulani wa mwaka fulani kwa zao fulani.

Kwa karne nyingi, wakulima hutumia viashiria vya asili kuamua wakati wa kupanda na baadhi ya viashiria ni pamoja na maua ya mimea pori na ndege wanaotengeneza viota. Viashiria hivi huamua jinsi msimu utakuwa mzuri kwa wakulima wa mazao fulani.

## **Uamuzi wa msimu**

Hali ya hewa inaweza kutabiriwa na hali ya mawingu pamoja na zana za kisasa kama vile Programu na mitandao ya kijamii. Viashiria vya asili ni muhimu kutabiri hali ya hewa kwa muda mrefu huku programu za mitandao za hali ya hewa zikifanya utabiri wa hali ya hewa kila siku.

Vile vile, taarifa husasishwa kila mara ikiwa una muunganisho wa mtandao, na utabiri kutoka kwa programu hizi ni sahihi zaidi ikiwa kuna kituo cha hali ya hewa karibu na kijiji. Programu ya simu ya mkononi ni bora zaidi kwani inatoa utabiri wa eneo lako.

Pakua Programu hiyo kutoka kwa play store, sakinisha, fungua na uchague eneo la sasa. Ili kuelewa nambari inayoshirikiwa na Programu, bonyeza ishara yenye nukta 3 upande wa juu kulia kwenye simu na uchague mm kwa mvua na km/saa kwa kasi ya upopo. Pia chagua mipangilio kisha chaguo la vizio, badilisha fahrenheit kuwa digrii sentigredi.

Hatimaye, kwenye skrini, maelezo ya hali ya hewa ya eneo la siku yanaonyeshwa, na pia hutoa taarifa ya hali ya hewa kwa siku 7 zijazo.